

Nambari ya Mtahiniwa \_\_\_\_\_

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

**MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA**

**SAYANSI JAMII**

PXVXKPF

110

**MUDA: SAA 2:30**

**ALHAMISI 17 OKTOBA, 2024 MCHANA**

**MAELEKEZO KWA MTAHINIWA**

1. Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C na D.
2. Jibu Maswali YOTE katika sehemu A, B na C. Jibu Maswali MANNE (4) kutoka sehemu D.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.
5. Majibu YOTE yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.
6. Simu ya mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.

KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI		
NAMBARI YA SWALI	ALAMA	SAINI
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
9.		
10.		
11.		
12.		
JUMLA		
SAINI YA MHAKIKI		



0102472

**Mtihani huu una kurasa 15 zenye maandishi**

**SEHEMU A: (Alama 20)**

**Jibu Maswali YOTE katika sehemu hii.**

1. Chagua jawabu sahihi katika vipengele ulivyopewa na andika herufi yake kwenye jadweli lililopo chini.
  - i. Ipi kati ya mahakama zifuatazo hutumika kutatua migogoro ya ndoa Zanzibar?

A. Mahakama ya Kadhi	B. Mahakama ya Mkoa
C. Mahakama ya Watoto	D. Mahakama ya Wilaya
  - ii. Jumuiya ya Afrika Mashariki ilianzishwa tena mwaka 2000. Kwa hivi sasa Jumuiya hiyo ina nchi wanachama wangapi?

A. 5	B. 6
C. 7	D. 8
  - iii. Umoja wa Mataifa umeanzishwa mwaka 1945. Ni miaka mingapi sasa tokea kuanzishwa kwake?

A. 69	B. 79
C. 89	D. 90
  - iv. Kati ya vyombo vifuatavyo, ni chombo kipi chenye mamlaka ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

A. Baraza la Manispaa
B. Baraza la Wawakilishi
C. Bunge
D. Mahakama
  - v. Baraza la Wawakilishi la Zanzibar limeanzishwa chini ya katiba ya Zanzibar ya mwaka gani?

A. 1964	B. 1979
C. 1984	D. 1990

- vi. Ipi kati ya orodha za nchi zifuatazo ni wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika?
- A. Angola, Lesotho, Tanzania, Malawi, Namibia
  - B. Lesotho, Malawi, Tanzania, Burundi, Uganda
  - C. Uganda, Angola, Kenya, Msumbiji, Zambia
  - D. Namibia, Kongo, Rwanda, Lesotho, Uganda
- vii. Ipi kati ya zifuatazo ni athari ya kiuchumi inayotokana na madawa ya kulevya?
- A. Husababisha hofu katika jamii
  - B. Kuenea huzuni kubwa nchini
  - C. Kupungua kwa nguvu kazi nchini
  - D. Kuwepo kwa uhalifu nchini
- viii. Moja kati ya athari chanya ya utandawazi Zanzibar ni
- A. Kudumaa kwa lugha yetu ya Kiswahili
  - B. Kuimarika kwa usafiri na mawasiliano
  - C. kuongezeka ukosefu wa ajira katika jamii
  - D. Mmong'onyoko wa maadili katika jamii
- ix. Katika nchi za kidemokrasia, mabadiliko ya uongozi wa nchi hufanyika kwa njia gani?
- A. Kura ya maoni
  - B. Mapinduzi
  - C. Uchaguzi mkuu
  - D. Urithi wa uongozi
- x. Mambo ambayo kila binadamu anastahili kuyapata bila ya kujali kabila, utaifa au jinsia yake huitwa
- A. Demokrasia
  - B. Haki za Binadamu
  - C. Utawala Bora
  - D. Utawala wa sheria

**JAWABU**

i.	ii.	iii.	iv.	v.	vi.	vii.	viii.	ix.	x.

2. Andika **Kweli** kwa maelezo yaliyo sahihi au **Si kweli** kwa maelezo yasiyo sahihi katika jadwali lililopo chini.
- i. Haki za kiraia na kisiasa ni haki za binadamu za kizazi cha pili.
  - ii. Chama cha ZPPP kilishiriki kwenye uchaguzi wa mwaka 1963 hapa Zanzibar.
  - iii. Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania huongozwa na Waziri Mkuu.
  - iv. Katika utekelezaji wa misingi ya utawala bora inapaswa kuzingatia haki za binadamu na utawala wa sheria.
  - v. Mahakama ya Wilaya huongozwa na Hakimu Mkaazi.
  - vi. Shindikizo kutoka kwa marafiki ni miongoni mwa sababu za utumiaji wa madawa ya kulevya.
  - vii. Umoja wa Mataifa ni jumuiya ya nchi masikini duniani.
  - viii. Sheria za madai zinarekebisha mwenendo wa raia mmoja na mwengine.
  - ix. Mfumo wa vyama vingi ni nyanja mojawapo ya utandawazi.
  - x. Jumuiya ya Madola ilianzishwa mwaka 1955.

**JAWABU**

i.	ii.	iii.	iv.	v.	vi.	vii.	viii.	ix.	x.

**SEHEMU B: (Alama 20)**

**Jibu Maswali YOTE katika sehemu hii.**

3. Jaza nafasi zilizowazi kwa kuandika jibu sahihi ulilopewa kwenye sanduku.

**Diwani, Donald Cameroon, 1964, Sheha, Fredrick Lugard, 1967, Ufaransa, 1974, Ujerumani, Nokoa, 1963, Uingereza, 1957**

- a. Mfumo wa utawala usio wa moja kwa moja barani Afrika ulisimamiwa na mtawala anaeitwa \_\_\_\_\_ na ule wa moja kwa moja ulisimamiwa na mtawala anaeitwa \_\_\_\_\_

## Nambari ya Mtahiniwa \_\_\_\_\_

- b. Katika harakati za kudai uhuru wa Zanzibar, vyama vya siasa vilishiriki katika chaguzi mbali mbali kuanzia mwaka \_\_\_\_\_ hadi mwaka \_\_\_\_\_
- c. Tanzania ilianzisha vijiji vya ujamaa mwaka \_\_\_\_\_ hadi mwaka \_\_\_\_\_ ili kuwaweka watu pamoja.
- d. Msaidizi wa Mwinyi Mkuu kwa upande wa Unguja alikuwa ni \_\_\_\_\_ na kwa upande wa Pemba alikuwa ni \_\_\_\_\_
- e. Mataifa ya Ulaya yaligombania sehemu mbalimbali za Afrika. Kwa mfano, Witu nchini Kenya iligombaniwa na taifa la \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_

4. Oanisha maelezo ya harakati za ukombozi kutoka **KIFUNGU A** na nchi inayokubaliana na malezo hayo kutoka **KIFUNGU B**. Andika herufi ya jawabu katika jadwali liliopo chini.

<b>KIFUNGU A</b>	<b>KIFUNGU B</b>
i. Vita vya msituni vilitumika kudai uhuru	A. Ghana
ii. Nchi ya kwanza kupata uhuru Afrika	B. Msumbiji
iii. Vita na njia ya mazungumzo zilitumika kudai uhuru	C. Tanganyika
iv. Nchi iliyoitawala Zimbabwe	D. Ufaransa
v. Nchi iliyoitawala Msumbiji kwa zaidi ya karne nne	E. Uingereza
	F. Ureno
	G. Zanzibar
	H. Zimbabwe

### JAWABU


<b>KIFUNGU A</b>	i.	ii.	iii.	iv.	v.
<b>KIFUNGU B</b>					

**SEHEMU C: (Alama 20)**

**Jibu Maswali YOTE katika sehemu hii.**

5. Jibu maswali yafuatayo kwa ufupi.
- a. Mzee Shingo ni mkulima wa siku nyingi anayelima mazao mbalimbali kama vile mihogo, mikarafuu, minazi na viazi vikuu. Bainisha mazao mawili (2) ya biashara yanayolimwa na mkulima huyo.
- i. \_\_\_\_\_
- ii. \_\_\_\_\_
- b. Kwanini sayari ya Venus huitwa nyota ya asubuhi?
- \_\_\_\_\_
- \_\_\_\_\_
- \_\_\_\_\_
- c. i. Bainisha bahari ndogo sana duniani.
- \_\_\_\_\_
- ii. Bainisha bahari kubwa sana duniani.
- \_\_\_\_\_
- d. Taja wilaya mbili (2) za Pemba.
- \_\_\_\_\_
- \_\_\_\_\_
- e. Taja visiwa viwili (2) vidogo vidogo vinavyopatikana katika kisiwa cha Unguja.
- i. \_\_\_\_\_
- ii. \_\_\_\_\_

6. Angalia kwa makini ramani iliopo chini kisha jibu maswali yanayofuata.



- a. Andika jina la ramani uliyopewa.  
\_\_\_\_\_
- b. Kwa kutumia alama hii ▲ , onesha sehemu ya Mlima Kilimanjaro kwenye ramani uliyopewa.
- c. Taja mikondo miwili (2) ya bahari iliyozunguka bara lililopo kwenye ramani uliyopewa.
- i. \_\_\_\_\_
- ii. \_\_\_\_\_
- d. Andika jina la mto mkubwa kabisa unaopatikana katika ramani uliyopewa.  
\_\_\_\_\_
- e. Jaza majina ya visiwa yaliyoainishwa kwa herufi **A** na **B** katika ramani uliyopewa.

**SEHEMU D: (Alama 40)**

**Jibu maswali MANNE (4) katika sehemu hii.**

7. Chambua sababu nne (4) zilizopelekea Zanzibar na Tanganyika kuungana na kuunda Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.
8. Jaalia wewe ni Sheha katika shehia ya Upendo ambapo vitendo vya ubaguzi na unyanyasaji wa kijinsia vimeshamiri. Chambua njia nne (4) utakazozitumia kupunguza vitendo hivyo katika shehia yako.
9. Mgogoro kati ya Ujerumani, Uingereza na Sultani wa Zanzibar ni chanzo cha kuibuka kwa Mkataba wa 1886. Eleza mambo manne (4) waliyoafikiana Uingereza na Ujerumani katika mkataba huo.
10. "Mara baada ya uhuru, mabadiliko makubwa yalifanyika katika utoaji wa huduma ya elimu katika Afrika huru". Thibitisha kauli hiyo kwa kueleza mabadiliko manne (4) ya kielimu yaliyofanyika baada ya uhuru.
11. Chambua athari nne (4) za kimazingira zinazotokana na uchimbaji wa mafuta ya petroli.
12. Jadili faida nne (4) za usafirishaji kwa nchi za Afrika Mashariki.

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---



**Nambari ya Mtahiniwa** \_\_\_\_\_

This image shows a blank sheet of white paper with horizontal ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There are no margins, text, or other markings on the paper.

**Nambari ya Mtahiniwa** \_\_\_\_\_

[illegible]

**Nambari ya Mtahiniwa** \_\_\_\_\_

[illegible]

**Nambari ya Mtahiniwa** \_\_\_\_\_

[illegible]

**Nambari ya Mtahiniwa** \_\_\_\_\_

[illegible]

**Nambari ya Mtahiniwa** \_\_\_\_\_

[illegible]

**Nambari ya Mtahiniwa** \_\_\_\_\_

[illegible]

